



MAISHA NA FALSAFA ZA SAFARI

*“Maisha ni mafupi, ila yana
safari ndefu ndani yake”*

Hazina Za Maisha Zilizofichika

DANIEL CHRISTOPHER ROBIN

KUHUSU MTUNZI



Daniel Christopher Robin ni mhitimu katika taaluma ya sayansi ya kompyuta na takwimu.

Ukiachilia mbali na taaluma ya sayansi ya kompyuta, **Daniel** pia ni **mwanaharakati** katika maisha na **mjasiriamali**, akiwa pia na taaluma nyingine alizozipata kupitia elimu binafsi katika kujifunza nadharia mbalimbali za kitaaluma, ujuzi na maarifa mbalimbali.

Kutokana na moyo na matamaniao ya kuwa mtu anayejitegemea, mwenye kutafuta uhuru wa kifikra, kiroho, kiuchumi, kuleta tofauti na kuwa hamasa na msaada kwa wengine katika jamii, hii imepelekea kufanya jitihada katika juhudi binafsi za mabadiliko katika kutengeneza jukwaa la kifursa.

Kupitia nguvu kubwa ya mabadiliko kuelekea njia ya mafanikio, na changamoto mbalimbali, uzoefu, maono na falsafa mbalimbali alizoziona na kujifunza katika maisha yake na maisha ya wengine pia, hii imepelekea kuweka mawazo mbalimbali katika sehemu moja ya kitabu *“Maisha na Falsafa za Safari.”*



+255 785 400 450



crobbiny@gmail.com



@danimzungupori



Dani Christopher Robin (@danimzungupori)



Dani Christopher Robin

ANGALIZO

Maandiko na maelezo yote yaliyotolewa na mwandishi katika toleo hili, hayatahusika na matokeo yoyote kwa msomaji au msikilizaji. Haya ni maono na mtazamo tu wa mtunzi kutoka sehemu mbalimbali, na kila mmoja anaweza kuwa na maono na mtazamo wa tofauti.

Yaliyomo ni uzoefu kutoka sehemu mbalimbali, kufundisha, kufungua uelewa, kutilia mkazo na kuhamasisha; na siyo kuchukuliwa kama kanuni na sheria za lazima za kuzifuata.

Kama tujuavyo, kila mmoja ana maono na mtazamo tofauti wa kimaisha, hivyo haufungwi na mtazamo ama maono na maoni ya mwingine.

Tambua kuwa, wewe ni mtu huru, na mwenye haki ya kuwa na fikra huru kimaisha.

Kimewezeshwa na JJR Company Ltd
S.L.P 2174 - Dodoma, Tanzania
<http://www.jjr.co.tz>

Copyright©2021
Haki zote zimehifadhiwa
ISBN 978-9976-88-674-0

*Hairuhusiwi Kutohoa, Kuiga, Kutoa Nakala, Kuzalisha,
Kuuza Au Kusambaza Nakala Hii Kwa Namna Iwayo Yoyote
Ile Pasipo Kibali Husika Cha Mhusika.*

YALIYOMO

SURA 1: SAFARI YA MAISHA	1
SURA 2: JUKWAA, NDOTO, NASAHA NA MAAMUZI	20
SURA 3: MAWAZO HAYAJI YAKIWA YAMEKAMILIKA	32
SURA 4: NYAKATI, VIKWAZO, MTAZAMO MPYA NA KUSUDIO LAKO	41
SURA 5: KUTOKA 57	58
SURA 6: MAISHA YANA SURA MBILI	73
SURA 7: WATU WANAOKUJA MAISHANI	86
SURA 8: UBONGO / AKILI NA UTASHI	98
SURA 9: UONGOZI / NGUVU YA MWENENDO	103
SURA 10: WAZAZI	115
SURA 11: DONDOO ZA NDOA NA MAHUSIANO	122
SURA 12: IMANI NA MUUMBA	149
SURA 13: KUSUDI LA MUNGU KWAKO	158
SURA 14: ULIMWEGU WA KANUNI NA TARATIBU	166
SURA 15: JICHO LA KIJASIRIAMALI	186

UTANGULIZI

“Maisha ni mafupi, ila yana safari ndefu ndani yake.”

“**Maisha na Falsafa za Safari,**” ni kitabu kinachoelezea safari ya maisha, changamoto mbalimbali, elimu, maarifa, ujuzi, uzoefu, kuhamasisha na kujengeana mitazamo chanya ya kukabili mambo na kusonga mbele katika kupambana kimaisha kwa matokeo chanya katika Ulimwengu huu wa kimwili na kiroho.

Kama ilivyo, maisha ni mafupi kwa namna ya muda tuliowekewa kuishi hapa duniani na namna ya mambo yaliyopo yanavyotukabili na kutupasa kuyatimiza kwa wakati. Wengine hudiriki kusema kuwa, “Muda hautoshi,” hasa kwa wale wengi walio na matumaini; yaani mambo ni mengi, lakini muda ni mchache huku tukizidi kunyauka.

Ila pia, pamoja na ufupi huo wa maisha, lakini ukija kuangalia namna ya baadhi ya mambo yalivyo magumu, pamoja na changamoto na mataabiko yaliyopo kwa baadhi ya watu, hufanya safari hii kwa wengine kuonekana ni ndefu sana, tena yenye dhiki na mataabiko, na kufikia kusema kuwa, “Muda hauendi, dunia imesimama na kuwaelemea,” hasa kwa wale waliokata tamaa na kupoteza matumaini.

Kitabu hiki kimegusia mambo mbalimbali katika safari hiyo, kama vile jinsi mwanadamu anavyosafiri katika safari hiyo, kuanzia kuzaliwa na kuja hapa duniani, utoto wake, kukua na ujana wake, mpaka anafikia uzeeni na kunyauka, pia changamoto mbalimbali anazokutana nazo kimaisha, imani, uchumi, ujasiriamali, utawala, maadili, malezi, makuzi, mahusiano, falsafa, elimu, ujuzi, majibu, hamasa na namna anavyokabili mazingira yake na jamii kwa ujumla.

Ni maneno yenye kufunza, kutoa elimu, maarifa, hekima, ujuzi, falsafa mbalimbali, kuhamasisha, kutia moyo na kutupatia ufunuo, taswira na dira mpya kimtazamo katika kukabiliana na mazingira yetu kimaisha, na kisha kusimama imara na kusonga mbele.